**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Manuals & Guidelines GePG

2017

# Waraka wa Hazina no.3 Kuhusu Mfumo Wa Serikali Wa Kielektroniki Katika Ukusanyaji Wa Mapato ya Serikali,2017

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/477

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Simu Nambari: 026-2963110
Nukushi: 026-2963109
Barua pepe: ps@mof.go.tz
Tovuti: www.mof.go.tz
[illegible] (Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe kwa Katibu Mkuu Hazina na siyo kwa mtu binafsi)

Jengo la "Treasury Square"
18 Barabara ya Jakaya Kikwete,
Sanduku la Barua 2802,
**40468 DODOMA,**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. CAB.481/558/01**

**4 Septemba, 2017**

Makatibu Wakuu Wote,
**TANZANIA BARA**

## WARAKA WA HAZINA NA. 3 KUHUSU KUTUMIA MFUMO WA SERIKALI WA KIELEKTRONIKI KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO YA SERIKALI (GOVERNMENT E-PAYMENT GATEWAY SYSTEM)

### 1.0 UTANGULIZI

Serikali inaendelea kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kujengwa kwa Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato yote ya Serikali. Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao imekamilisha utengenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali ujulikanao kama "Government e-payment Gateway System" "GePG". Lengo la mfumo huo ni kuongeza tija na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi zote za Serikali.

### 2.0 UTENGENEZAJI NA UUNGANISHWAJI WA MFUMO

Mfumo huo umezingatia mahitaji halisi ya Serikali katika Mifumo ya kielektroniki (Business requirements) pamoja na taratibu zote za kitaalamu. Baada ya kutengenezwa kwa mfumo wa GePG, Serikali ilifanya majaribio kuanzia Juni, 2017 hadi Julai, 2017 ambapo umethibitika kufanya kazi

vizuri na kukidhi mahitaji yaliyotarajiwa. Mfumo huu tayari umeunganishwa na ofisi mbalimbali zinazokusanya mapato ya Serikali ikiwemo Wizara ya Aridhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, Wizara ya Nishati na Madini, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Wakala wa Misitu. Ofisi zinazoendelea kuunganishwa ni pamoja na Wizara ya Kazi Vijana Ajira na Wenye Ulemavu, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi pamoja na taasisi nyingine za Serikali.

Ili kuleta tija na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali Mfumo wa GePG umeunganishwa na taasisi zinazotoa huduma za fedha kama vile benki za NMB na CRDB pamoja na Kampuni za simu ambazo zimeanza kutoa huduma kupitia matawi, mawakala na mitandao ya simu. Hivyo, timu ya wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea na uunganishaji wa mfumo wa GePG kwa wadau wengine wanaoweza kurahisisha ukusanyaji wa mapato pamoja na ofisi za Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi nyingine za Serikali ili kuendelea kukusanya mapato kwa kutumia mfumo huu. Hivyo, kila Afisa Masuuli anayekusanya mapato ya Serikali anasisitizwa kuhakikisha ofisi yake imeunganishwa kwenye mfumo wa GePG na watumishi wanaohusika wanapewa mafunzo yanayostahiki mapema iwezekanavyo ili kukusanya mapato yote kwa ukamilifu.

## 3.0 MATAKWA YA SHERIA YA KUTUMIA MFUMO WA GePG

Bunge lilipitisha kifungu cha 44 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 (The Finance Act, 2017) na kufanyia marekebisho Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kwa kuanzisha mfumo huu wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali "Government e-payment Gateway System". Aidha, Sheria imeweka sharti kwa Wizara na Taasisi za Serikali kutumia mfumo huu kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato. Vile vile, Maafisa Masuuli wamewekewa sharti la kuhakikisha kwamba mapato yote katika Taasisi wanazozisimamia yanakusanywa kupitia Mfumo huu. Hivyo, kila Afisa Masuuli wa Wizara na Taasisi zote za Serikali zinazokusanya mapato anakumbushwa kuanza kutekeleza Sheria hiyo mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha mfumo wa GePG unatumika kikamilifu katika ukusanyaji wa mapato yote ya fungu lake kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa Sheria.

## 4.0 HITIMISHO

Kutokana na kukamilika kwa Mfumo huu wa GePG ambao uliagizwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba uanze kutumika mwaka 2017/18, Wizara ya Fedha na Mipango inawajulisha kuwa tayari Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 imeanza kutekelezwa ikiwemo Sharti la kuwataka Maafisa Masuuli wa Wizara na Taasisi za Umma kutumia Mfumo huu wa GePG katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, ninawajulisha rasmi kupitia Waraka huu, kuhakikisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali zote zinatumia Mfumo huu wa GePG katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali kuanzia mwezi Agosti, 2017. Aidha, kwa Maafisa Masuuli ambao Ofisi zao bado hazijaunganishwa kwenye mfumo huu mnaelekezwa kuwasiliana na Mkurugenzi wa Mifumo ya Fedha, Wizara ya Fedha na Mipango kwa simu namba +255 22 212 9697 au kwa barua pepe: gepg@mof.go.tz.

Doto M. James
**KATIBU MKUU HAZINA NA**
**MLIPAJI MKUU WA SERIKALI**

**Nakala:** Katibu Mkuu Kiongozi,
Ofisi ya Rais,
IKULU,
S.L.P 9120,
**DAR ES SALAAM.**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
**DAR ES SALAAM.**

Msajili wa Hazina,
Jengo la CHC,
Mtaa wa Mirambo,
S.L.P. 3193,
**DAR ES SALAAM.**